# BRELA

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**

ISSN: 000401|Toleo Na. 06| Julai – Septemba, 2023




# BRELA NA URAHISISHAJI HUDUMA KWA WAFANYABIASHARA

# YALIYOMO


4 Rais Mwinyi aikabidhi BRELA tuzo ya ushindi





6 Wabunifu Sekta ya Kilimo Wasaidiwe - Mpango





8 Taasisi za Udhibiti zaelekezwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara






12 Fanyeni kazi kwa bidii – Nyaisa




BRELA
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

# Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu



*Bw. Godfrey Nyaisa*
*Afisa Mtendaji Mkuu BRELA*

Nafurahi kuwasilisha toleo hili la sita ambalo ni mwendelezo wa majarida yanayotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). Toleo hili limesheheni maelezo na taarifa mbalimbali za shughuli kama zilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Taasisi kwa kadri ya maboresho yanayoendelea kuimarisha utoaji wa huduma.

Kupitia Jarida hili ni dhahiri wadau watapata fursa ya kufahamu na kuelewa hatua zinazochukuliwa na BRELA kuhakikisha huduma zinaboreshwa na kupatikana kwa urahisi.

Katika kipindi cha matayarisho ya Jarida hili, BRELA imeshuhudia na kushiriki katika matukio mbalimbali yaliyowezesha kuipa nafasi ya kukutana na wadau wake kuweza kupata uzoefu na kubadilishana mawazo, lengo likiwa ni kuimarisha mifumo inayomwezesha mwananchi kurasimisha shughuli zake na kuzipa uhai wa kisheria. Aidha, BRELA kupitia vikao vya mashauriano, ilipata nafasi ya kukutana na Taasisi za Fedha, Uchunguzi pamoja na Mamlaka za Udhibiti na kujadili namna bora ya kushirikiana na kuwezesha wadau na wananchi kwa ujumla kufanya biashara kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Pia BRELA ilipata fursa ya kutoa mafunzo kwa mara ya kwanza kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Juhudi za kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili na weledi, BRELA iliendesha mafunzo kwa maafisa wake kuhusu namna ya kuandaa mashauri mahakamani na kutoa ushahidi wa kesi mbalimbali zinazohusisha Taasisi.

Aidha, watumishi pia wamepata fursa ya mafunzo kuhusu huduma za uwekezaji katika mifuko inayosimamiwa na serikali kwa ajili ya kuboresha ustawi wa maisha yao wakiwa katika utumishi na baada ya kustaafu.

BRELA imeshiriki katika maonesho ya kitaifa na kimataifa ambayo ni pamoja na ushiriki katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam maarufu kama Saba Saba ambapo iliibuka na ushindi wa nafasi ya kwanza katika kipengele cha Uwezeshaji wa Ukuzaji wa Biashara na Uwekezaji yaliyofanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwalimu J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam. Matokeo haya ni kielelezo thabiti kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa na Wakala na imani waliyonayo wadau kutokana na huduma zinazotolewa na Taasisi. Maonesho mengine ni pamoja na Maonesho ya Kilimo na Mifugo maarufu kama NaneNane yaliyofanyika jijini Mbeya, Maonesho ya Teknolojia ya Madini, Geita, pamoja na Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza.

Kwa ujumla, taarifa zilizomo katika Jarida hili ni za utekelezaji wa majukumu ya BRELA kupitia Kurugenzi, Idara na Vitengo vyake. Miongoni mwa yaliyotekelezwa ni pamoja na kuhamasisha na kutoa elimu kupitia ushiriki wa mikutano, maonesho na kufanya kampeni za ukaguzi elimishi mtaa kwa mtaa, kutoa elimu na mafunzo kwa makundi mbalimbali wakiwemo wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo, kuandaa machapisho na makala mbalimbali kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Aidha, katika toleo hili mikakati mbalimbali imeainishwa na jinsi ya kutatua changamoto za kiutendaji zikiwemo zile za kimfumo na kitaasisi kwa lengo la kujenga mazingira bora na wezeshi ya kibiashara kwa kushirikisha wadau ambao ni pamoja na Taasisi za Udhibiti, Taasisi za Fedha na zile za Uchunguzi kupitia vikao vya mashauriano. Hivyo, naomba tuungane kwa pamoja katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli zetu kidigitali na kufanikisha urasimishaji ili kuzipa biashara za wananchi uhai wa kisheria. Tunakutakia usomaji mwema wa Jarida hili.


## BODI YA UHARIRI

**Andrew Mkapa**
**Mwenyekiti**

**Wajumbe**

Meinrad Rweyemamu
Tawi Kilumile
Abdulrahman Songoro
Neema Kitala
Tulizo Mpina
Alpha Nuhu
Yusuph Nakapala

**Roida Andusamile**
**Katibu**

# Rais Mwinyi aikabidhi BRELA tuzo ya ushindi




***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akikabidhi tuzo ya mshindi wa kwanza katika kipengele cha Uwezeshaji wa Ukuaji wa Biashara na Uwekezaji kwa mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu Bw. Andrew Mkapa wakati wa ufungaji wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) katika Viwanja vya Mwalimu J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.***

***Na Gloria Mbilimonywa***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha Uwezeshaji wa Ukuzaji wa Biashara na Uwekezaji na kuibuka mshindi wa nne katika kipengele cha Banda Bora katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam yaliyofanyika katika uwanja wa Mwalimu J.K Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

Tuzo za ushindi huo zilitolewa tarehe 13 Julai 2023 na Rais



***Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi aikabidhi BRELA tuzo ya udhamini wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, kwa Bw. Andrew Mkapa Mkurugenzi wa Leseni, BRELA. aliye mwakilisha Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi.***

wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, wakati wa kufunga maonesho hayo.

Katika kipengele cha Uwezeshaji wa Ukuzaji wa Biashara na Uwekezaji waliochukua nafasi ya pili ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakifuatiwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA). Kwa upande wa mabanda bora waliochukua nafasi ya kwanza ni banda la Algeria, ikifuatiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) nafasi ya tatu ilichukuliwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT).

Ushindi wa nafasi ya kwanza kwa BRELA ni mwendelezo wa jitihada za Taasisi katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau wake, ambapo katika Maonesho ya 46 BRELA ilipata ushindi wa nafasi ya pili katika kipengele hicho hicho cha Uwezeshaji wa Ukuzaji wa Biashara na Uwekezaji.

Kabla ya kufunga Maonesho hayo, Rais Mwinyi alitembelea Banda la BRELA ambapo alipata fursa ya kuona jinsi Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS) unavyofanya kazi. Pia alitumia nafasi hiyo kukabidhi cheti cha Usajili kwa mmoja wa wafanyabiashara waliofika katika Banda la BRELA na kupata huduma ya usajili wa papo kwa papo zilizotolewa wakati wa Maonesho hayo.



***Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akipata maelezo ya namna Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS) unavyofanyakazi kutoka kwa Bw. Andrew Mkapa aliyemwakilisha Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA wa alipotembelea banda la Taasisi hiyo kwenye Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam alipofunga maonesho hayo.***



***Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi wa akimkabidhi mfayabiashara cheti cha usajili wa Jina la Biashara alipotembelea banda la BRELA wakati wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam.***

# Wabunifu Sekta ya Kilimo Wasaidiwe - Mpango

*Na Roida Andusamile*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amezitaka wizara na taasisi husika kuhakikisha wabunifu katika Sekta ya Kilimo wanatambuliwa na kulindwa kisheria ili waweze kunufaika.

Mhe. Dkt. Mpango alitoa agizo hilo tarehe 1 Agosti, 2023 alipokuwa akifungua Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima maarufu kama Nane Nane yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Mhe. Mpango alisema, yanapofanyika Maonesho haya ni muhimu kuwatambua wabunifu katika Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ikiwa ni njia mojawapo ya kuwahamasisha na kuwasaidia kulinda ubunifu wao kisheria.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi katika ufunguzi wa maonesho hayo Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe alisema umefika wakati sasa kwa bidhaa zote za chakula na mbegu kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi zitambulike kwa kuhusisha masuala ya Miliki Ubunifu tofauti na ilivyo sasa.



***Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akihutubia wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya Wakulima Nane Nane jijini Mbeya.***

Alisema Tanzania ina utajiri wa mazao mengi ya chakula pamoja na mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na vituo vya utafiti vya hapa nchini lakini vinaposafirishwa nje ya nchi havitambuliki kama asili yake ni Tanzania, hivyo suala la Miliki ubunifu ni muhimu kulizingatia.

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ambayo ina dhamana ya kusajili Miliki Ubunifu, ilishiriki katika maonesho hayo. Mbali na kuhamasisha urasimishaji wa biashara, BRELA ilitumia fursa ya maonesho hayo kuwatembelea wabunifu mbalimbali na kuwapatia elimu kuhusu umuhimu wa kusajili BRELA vumbuzi zao ili ziweze kulindwa kisheria.

Kwenye maonesho hayo yaliyohitimishwa tarehe 8 Agosti, 2023, yenye kauli mbiu "Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula", BRELA ilitoa huduma za papo kwa papo za sajili pamoja na kutoa elimu kwa wadau waliotembelea mabanda yake.

> *"Nimefurahi kumuona mbunifu ambaye ameunda gari inayopukuchua mahindi na bidhaa zingine, mbunifu kama huyu anapaswa kusaidiwa ili anufaike na ubunifu wake".*

# Taasisi za Fedha zatakiwa kukusanya,kutunza taarifa za Wamiliki Manufaa

*Na Theressa Chilambo*

Taasisi za Fedha nchini zimehimizwa kuisaidia Serikali kukusanya na kutunza taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni kwa kuwa wao wanazitambua kwa kupitia huduma mbalimbali za kifedha wanazozitoa hapa nchini. Nia ni kufichua maovu yanayofanyika nyuma ya kampuni.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo wakati akifungua warsha ya siku mbili (2) ya utoaji elimu kwa Taasisi za Fedha juu ya dhana ya umiliki manufaa, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Warsha hii ilifanyika Julai, 2023 katika Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.

"Changamoto za taarifa za wamiliki baadhi walikuwa wanatumia Kampuni kukwepa kodi, kupitisha fedha haramu, ugaidi na Serikali imeona iwe na uhakika wa kupata taarifa za wenye kampuni hivyo kuwa na ulazima wa kukutana na Taasisi za Fedha", alisema Mhe. Mpogolo.

Mhe. Mpogolo alisema jitihada za serikali haziwezi kufanikiwa bila Taasisi za Fedha, kwa kuwa ni muhimu. BRELA ni kiungo kati ya maelekezo, maagizo na sheria mbalimbali za Serikali lakini mtekelezaji wa sheria hii ni Taasisi za Fedha. Ili kufanikiwa, Serikali inahitaji kushirikiana nanyi kwa ajili ya kutimiza utekelezaji wa sheria iliyopitishwa.

Naye, Bw. Andrew Mkapa, Mkurugenzi wa Leseni kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA alisema kuwa Taasisi hushirikiana kwa karibu na Taasisi za Fedha katika utendaji kazi wa kila siku hivyo ni matarajio yake kuwa warsha juu ya dhana ya Umiliki Manufaa itaimarisha mshikamano. Aliongeza kuwa BRELA itapata ushirikiano utakaozalisha ufanisi, kuibua michango mizuri yenye kujenga na kupata uelewa wa pamoja kwa manufaa ya wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi kwa ujumla.

Bw. Mkapa alisisitiza kwamba BRELA imeona umuhimu mkubwa wa kutoa elimu kwa taasisi za fedha kutokana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 iliyopitisha marekebisho ya Sheria ya Kampuni Sura 212 nakanuni zake kupitishwa na Waziri mwenye dhamana na biashara nchini.

> *"Changamoto za taarifa za wamiliki baadhi yao walikuwa wanatumia Kampuni kukwepa kodi, kupitisha fedha haramu, ugaidi na Serikali imeona iwe na uhakika wa kupata taarifa za wenye kampuni hivyo kuwa na ulazima wa kukutana na Taasisi za Fedha".*

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji kutoka Chama cha Mabenki Tanzania (TBA) Bi. Tusekelege Mwaikasu alisema kuwa warsha hiyo imekuwa ya umuhimu mkubwa kwao kwa sababu ni sheria ambayo imewekwa kama mwongozo. Aliongeza kuwa jukumu lao ni kutekeleza kwa kutoa taarifa zenye mashaka au matendo tofauti ya mtumiaji wa akaunti na kuwasaidia kujua mmiliki halali wa Kampuni husika iliyofungua akaunti kwenye benki hiyo.

BRELA iliratibu warsha ya siku mbili kwa Taasisi za Fedha ili kuwajengea uelewa juu ya dhana ya Mmiliki Manufaa wa Kampuni ambapo mmiliki anatambulika moja kwa moja au kwa kupitia mtu mwingine mwenye zaidi ya asilimia tano (5%) ya uwekezaji au ufanyaji maamuzi kwenye Kampuni.



***Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mhe. Edward Mpogolo (aliyeketi wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa warsha kuhusu dhana ya umiliki manufaa kutoka Taasisi za Fedha iliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), jijini Dar es Salaam.***

# Taasisi za Udhibiti zaelekezwa kuweka mazingira wezeshi ya biashara

*Na Theresa Chilambo*

Taasisi za Udhibiti zimeelekezwa kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara nchini ikiwa ni jukumu kuu na la msingi ili kutatua kero za wafanyabaishara na wawekezaji kwenye sekta mbalimbali na sio kuwa kikwazo na endapo kuna sheria, kanuni na taratibu zenye mikinzano zirekebishwe.

Wito huo ulitolewa na Dkt Hashil Abdallah, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara alipokuwa akifunga kikao kazi kilichohudhuriwa na Taasisi za Udhibiti tarehe 15 Septemba, 2023 mjini Morogoro ambapo kikao hicho kiliratibiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Dkt. Abdallah alisema kuwa taasisi za kiserikali zinatakiwa kuzungumza kimifumo hasa katika maeneo yanashabihiana ili kumsaidia ambaye anataka kufanya baishara au kuwekeza nchini apate huduma kwa kasi kwakuwa uchumi wa nchi unakuwa kwa kutegemea



***Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt Hashil Abdallah akizungumza na washiriki kutoka Taasisi za Udhibiti wakati akifunga kikao kikao mjini Morogoro.***

mazingira bora ya ufanyaji biashara nchini na huchochewa kuanzia ngazi ya Taasisi.

"Tuhakikishe uwezeshaji wetu unaendana na kasi ya utatuzi wa kero zinazozungumziwa, ni jukumu letu kuzitatua na Wizara yetu ambayo imepewa dhamana ya kusimamia sekta hii pamoja na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kuzipatia




***Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Abdallah akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa kikao kazi cha Taasisi za Udhibiti baada ya kufunga rasmi kikao hicho tarehe 15 Septemba, 2023 kilichofanyika mjini Morogoro.***



***Baadhi ya washiriki kutoka Taasisi za Udhibiti wakishiriki kikao kazi kilichoandaliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) mjini Morogoro.***

ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoathiri uanzishwaji na ufanyaji wa biashara", alieleza Dkt. Abdallah

Aliendelea kusema kuwa Wizara kupitia Taasisi zake itaendelea kukutana mara kwa mara na wadau wa Sekta hii hususan wafanyabiashara ili kupokea changamoto zao pamoja na kuwapatia mrejesho wa hatua mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali kuboresha sekta hii.

Dkt. Abdallah alisisitiza kuwa ili kufanikisha utekelezaji wa azma ya Serikali ya Awamu ya Sita Wizara ya Viwanda na Biashara inatekeleza maono hayo kwa vitendo kwa kufanya mapitio ya Sera zake hususan Sera Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 ambayo kwa sasa iko katika ngazi ya Baraza la Mawaziri ambapo mapitio ya Sera hii yamezingatia wakati wa sasa wa ufanyaji biashara, mabadiliko ya sayansi na teknolojia

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa, alimhakikishia Katibu Mkuu kuwa BRELA itawasilisha rasmi maazimio yote ya kikao ili kuweza kuchukua hatua mbalimbali za maeneo ambayo yanahitaji uboreshaji na kufikiwa maamuzi kwa haraka.

> *"Tuhakikishe uwezeshaji wetu unaendana na kasi za utatuzi wa kero zinazozungumzwa, ni jukumu letu kuzitatua na Wizara yetu ambayo imepewa dhamana ya kusimamia sekta hii pamoja na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoathiri uanzishwaji na ufanyaji wa biashara".*

Aliongeza kwa kusema kuwa mageuzi yanayofanywa na Serikali, yanalenga pia kuwawezesha wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara kuzifikia fursa mbalimbali za masoko ya Kikanda na Kimataifa ili kukuza mauzo ya nje na kuiwezesha nchi kuongeza wigo wa ajira na fedha za kigeni pamoja na malengo ya Jumuiya mbalimbali za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania imeridhia kuwa mwanachama.

Akifungua Kikao Kazi kati ya BRELA na Taasisi za Udhibiti, tarehe 13 Septemba, 2023, katika ukumbi wa Nashera mjini Morogoro, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa, alieleza kuwa ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ni vyema kujadili kwa pamoja changamoto na vikwazo vinavyosababishwa



***Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akizungumza na washiriki wakati wa ufunguzi wa kikao kazi baina ya BRELA na Taasisi za Udhibiti kilichofanyika tarehe 13 Septemba, 2023 mjini Morogoro.***

na usimamizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotumika na kuangalia jinsi ya kuvikwamua, ili kukuza uchumi wa Tanzania.

"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kuinua hali ya uchumi wa nchi, hivyo BRELA katika kuunga mkono jitihada hizo, inakutana nanyi ili kujadili mikinzano na muingiliano katika utoaji wa huduma na jinsi ya kuondokana na hali hiyo ili hatimaye kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa Tanzania hawakumbani na changamoto au uchelewaji wa kupata huduma hapa nchini", alisema Bw. Nyaisa.

Alitoa mfano kuwa BRELA imekuwa ikikutana na changamoto katika utendaji na kusababisha usumbufu kwa wateja, pale ambapo taasisi za udhibiti zimekuwa zikitoa vibali vya biashara bila kujiridhisha endapo mfanyabiashara huyo amesajili Kampuni au Jina la Biashara. Aliongeza kwa kusema kuwa athari kubwa anayoweza kuipata mfanyabiashara huyo endapo atapatiwa kibali wakati hajasajili Kampuni au Jina la Biashara ni kushindwa kusajili Jina la Biashara au Kampuni endapo jina husika litakuwa na ufanano na majina yaliyosajiliwa BRELA, hivyo mhusika kulazimika kubadilisha jina husika.

Aliendelea kusema kuwa athari kubwa anayoipata mfanyabiashara anaposhindwa kusajili jina linaloonekana kwenye kibali alichokipata, huathiri biashara yake ikiwa ni pamoja na kukosa zabuni, mikopo au kuingia mikataba na taasisi za umma. Hii ni kwa kuwa usajili wa Jina la Biashara au Kampuni ni hitaji la msingi katika mfumo wa sasa wa Ununuzi unaosimamiwa na PPRA uitwao NEST, ambao




***Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akiwa pamoja na maafisa waandamizi kutoka BRELA pamoja na mwakilishi kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara wakati wa kikao kazi cha taasisi za udhibiti kilichoandaliwa na BRELA na kufanyika mkoani Morogoro.***



***Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Taasisi za Udhibiti wakimsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara akifunga kikao hicho.***

> *"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kuinua hali ya uchumi wa nchi, hivyo BRELA katika kuunga mkono jitihada hizo, inakutana nanyi ili kujadili mikinzano na muingiliano katika utoaji wa huduma na jinsi ya kuondokana na hali hiyo ili hatimaye kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa Tanzania hawakumbani na changamoto au uchelewaji wa kupata huduma hapa nchini".*

umeunganishwa na Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS) wa BRELA. Katika mfumo huu, mfanyabiashara hataweza kujisajili katika mfumo wa NEST iwapo hajasajili Kampuni au Jina la Biashara.

Naye, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Bw. Lazaro Msasalaga, alisema kuwa kikao kazi hicho ni muhimu maana kinatekeleza malengo ya BluePrint kwa kuzingatia umuhimu wa wafanyabiashara kuwa na Leseni ya Biashara inayotolewa na BRELA na leseni zingine zinazotolewa na Taasisi za Udhibiti ikizingatiwa kuwa sheria hizo zilikuwepo kabla ya andiko hilo.

Washiriki wa Kikao Kazi hicho kutoka Taasisi za Udhibiti ambao ni wanasheria pamoja na maafisa wanaohusika na utoaji wa vibali mbalimbali, wamepata fursa ya kujadiliana kwa siku tatu na kutoa maazimio ambayo yatawasilishwa ngazi za juu kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

BRELA, ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kuzinduliwa rasmi tarehe 3 Desemba, 1999 ikiwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Majukumu ya BRELA ni pamoja na Kusajili majina ya Biashara, Kampuni, Alama za Biashara na Huduma, Utoaji wa Hataza, Utoaji wa Leseni za Biashara Kundi "A" na Utoaji wa Leseni za Viwanda na Vyeti vya Usajili wa Viwanda.



***Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Taasisi za Udhibiti wakimsikiliza Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA akitoa neno la ukaribisho wakati wa kikao hicho.***

# Fanyeni kazi kwa bidii – Nyaisa



***Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa, akizungumza na watumishi wa BRELA katika Makao Makuu ya Ofisi za Taasisi hiyo baada ya kukabidhiwa tuzo ya ushindi wa kwanza katika kipengele cha Uwezeshaji wa Ukuaji wa Biashara na Uwekezaji wakati wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam.***

***Na Gloria Mbilimonywa***

Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa, amewataka watumishi wa BRELA kuutumia ushindi walioupata katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kuwa ni chachu ya kufanya kazi kwa bidii na mshikamano.

Bw. Nyaisa alitoa wito huo tarehe 17 Julai, 2023 katika Ofisi za BRELA Makao Makuu baada ya kukabidhiwa tuzo za ushindi na Mkurugenzi wa Leseni Bw. Andrew Mkapa aliyezipokea kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Mwinyi wakati wa kufunga Maonesho hayo Julai 13, 2023 katika Uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Wilaya ya Temeke Jijini Dar es Salaam.

Bw. Nyaisa alisema kwa miaka mitatu mfululizo BRELA imekuwa ikipata ushindi katika kipengele cha Uwezeshaji na Ukuzaji wa biashara na uwekezaji, kwani katika Maonesho ya 45 ilipata ushindi wa tatu, katika Maonesho ya 46 ushindi wa pili na kwa mwaka huu katika Maonesho ya 47 imepata ushindi wa kwanza. Hivyo, jitihada zaidi zinahitajika ili kuendelea kuwa washindi na hata ikiwezekana kuwa washindi wa jumla wa maonesho yanayofuata.

"Nimefurahi BRELA kuwa washindi wa kwanza katika kipengele cha uwezeshaji na Ukuzaji wa biashara na uwekezaji na ushindi huu umeleta hamasa kwa Taasisi nyingine kutaka kufahamu mkakati uliowezesha kuendelea kutwaa ushindi huu. Nina imani kuwa ni Umoja wetu ndiyo uliotufikisha hapa", alifafanua Bw. Nyaisa.

Hata hivyo, aliwataka watumishi kutobweteka na ushindi huo bali kujipanga zaidi ili kuhakikisha kuwa BRELA inaendelea kufanya vizuri katika kipengele hicho, ikiwa ni pamoja na kufanya kazi kwa bidii, kutoa huduma bora na kuwajali wateja wakati wote.

Aidha, Bw. Nyaisa alisisitiza kuwa ili kuendelea kung'ara na kutunza taswira ya Taasisi, watumishi wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na kila mmoja kuelewa kuwa asipofanya kazi vizuri ataathiri wengine. Hivyo, ni lazima kila mmoja kujitambua na kufahamu kuwa kazi anayoifanya ina mchango mkubwa na

*"Tunapaswa kuepuka urasimu usio wa lazima katika utendaji wa kazi na utoaji wa huduma zetu ili kukidhi matakwa ya wateja wakati wote ambao ni sekta ya umma na sekta binafsi ".*




***Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akipokea cheti cha Udhamini kutoka kwa Mkurugenzi wa Leseni Bw. Andrew Mkapa kilichotolewa wakati ufungaji wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam.***

asipoifanya vizuri ina athari kwa mwingine.

Vile vile aliwaasa watumishi kuwa na nidhamu, kwa kuwa nidhamu ndio msingi mkuu katika utendaji kazi na kila mmoja aheshimu nafasi aliyopewa katika utumishi wake na kwamba njia bora kwa BRELA kuonekana inajali wateja na inahudumia wateja wake ni kuhakikisha inatoa suluhu ya maswali na mahitaji yao kwa wakati.

"Tunapaswa kuepuka urasimu usio kuwa wa lazima katika utendaji wa kazi na utoaji wa huduma zetu ili kukidhi matakwa ya wateja wakati wote ambao ni sekta binafsi na ya umma", alisisitiza Bw. Nyaisa.

Kwa ujumla, Bw. Nyaisa aliwapongeza watumishi wote pamoja na timu iliyoshiriki katika maonesho na kuwahakikishia kuwa ushindi huo ni wa watumishi wote kwani kila mmoja kwa nafasi yake amechangia na kuhakikisha kuwa ushindi umepatikana. Hivyo, watumishi waendelee kufanya kazi kwa bidii zaidi na kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Mbali ya kupata ushindi wa kwanza, BRELA pia ilipokea cheti cha ushindi wa nne wa jumla katika mabanda bora pamoja na tuzo ya kutambuliwa kwa mchango wa waliodhamini Maonesho ya mwaka 2023.



***Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Taasisi hiyo baada ya kuzipokea tuzo zilizotolewa kufuatia ushindi wa nafasi ya kwanza katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam.***






# BRELA mtaa kwa mtaa ukaguzi elimishi

*Na Sheila Mfunami*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewahimiza wafanyabiashara katika eneo la Buguruni, Wilaya ya Ilala, kurasimisha biashara zao ili kuwa na utofauti kati ya biashara moja na nyingine.

Wito huo ulitolewa tarehe 26 Julai, 2023 na Afisa Usajii wa BRELA Bw. Yusuf Mwasakafyuka wakati wa ukaguzi elimishi kwa wafanyabiashara waliokuwa wakipata elimu kuhusu huduma



zinazotolewa na BRELA katika maeneo ya Buguruni kwa Mnyamani.

Akizungumza na wafanyabiashara hao Bw. Mwasakafyuka alisema zoezi hilo limelenga katika kutoa elimu na kuhimiza kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara.

"Lengo kuu ni kuwapa elimu wafanyabiashara ambao bado hawajasajili biashara zao na wale ambao wamesajili ili watekeleze matakwa ya kisheria baada ya usajili", alisema Bw. Mwasakafyuka.

Pia alitumia fursa hiyo kuwasikiliza na kupokea changamoto wanazokumbana nazo wakati wa kupata huduma za BRELA kupitia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao.

Ukaguzi huu elimishi uliofanyika katika wilaya zote za Jiji la Dar es Salaam ambazo ni Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo na Kigamboni.




*Maafisa wa Wakala wa BRELA wakipita mtaa kwa mtaa katika maeneo mbalimbali ya wilaya za mkoa wa Dar es Salaam wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi juu umuhimu wa kurasimisha biashara.*






# Mtaa kwa mtaa ya BRELA yamfikia msanii Barnabas

*Na Sheila Mfunami*

Hatimaye mwanamuziki na Mkurugenzi wa Hightable Sound Entertainment, Bw. Elias Barnabas maarufu kama 'Barnaba Classic', amefanikiwa kusajili Jina la Biashara la "Poa Water", ambalo atalitumia katika biashara yake ya maji.

Mwanamuziki huyo amepata huduma ya papo kwa papo baada ya kutembelewa ofisini kwake na maafisa wa BRELA waliopo katika zoezi la ukaguzi elimishi ambapo huwatembelea wadau mtaa kwa mtaa.

Aidha, BRELA inaendelea na jitihada za kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa kutoa huduma zake za kurasimisha biashara kupitia Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS).




*Msanii Bw. Elias Barnabas maarufu kama Barnaba Classic akiwa ameshika cheti cha usajili baada ya kusajili Jina la Biashara la "Poa Water" wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi liloendeshwa na BRELA katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.*



*Msanii Elias Barnabas maarufu kama Barnaba Classic akipokea cheti cha usajili wa Jina la Biashara kutoka kwa Afisa wa BRELA Bi. MaryGlory Mmary wakati wa zoezi la ukaguzi elimishi uliofanywa na BRELA katika mitaa mbalimbali Jijini Dar es Salaam.*

# BRELA yatakiwa kuendelea kuboresha huduma

*Na Mwandishi wetu*

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alieleza kuwa licha ya kuwapo kwa changamoto ya mtandao katika kufanya usajili kwa njia ya mtandao lakini kuna maboresho makubwa yaliyofanywa na Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

Pia aliitaka BRELA kuendelea kushirikiana na taasisi nyingine lengo likiwa ni kurahisisha utoaji huduma zake na kuwapo kwa mabadiliko ya mifumo mbalimbali ukiwemo mfumo mpya wa Tausi.

Naibu Waziri huyo aliyasema hayo jijini Mbeya tarehe 5 Agosti, 2023 alipotembelea banda la BRELA katika maonesho ya Nane Nane ya Wakulima na Wafugaji, ambayo yaliofanyika Kitaifa jijini Mbeya katika viwanja vya John Mwakangale yenye kauli mbiu isemayo 'Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo Endelevu ya Chakula'. Alieleza kuwa malalamiko makubwa yako kwenye leseni Daraja B ambazo zinatolewa na Halmashauri.

Aidha, aliitaka BRELA kuendelee kuboresha mifumo ili wananchi wasipate vikwazo katika kufanya biashara zao.

"Tuangalie namna ya kuiboresha mifumo yetu ili isomane na Taasisi nyingine mtu anapotaka kuingia kwenye mfumo aone na taasisi nyingine anayotaka," alisema Kigahe.

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano BRELA, Bi. Roida Andusamile, alisema kuwa Wakala ina mpango wa kuoanisha mifumo yake na mingine ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

"Kuna mpango ambao utatuwezesha ili mifumo hii iweze kusomana na ikisomana urasimu utaondoka kwa watu tunaowahudumia," alisema.

> *"BRELA kaeni na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ili muone changamoto hii mnaitatuaje, hiki ni kilio cha wafanyabiashara ambao matarajio yao makubwa kwa Serikali ni kuwaondolea urasimu usiokuwa wa lazima".*




***Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) akisalimiana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bi. Roida Andusamile alipotembelea banda la BRELA wakati wa Maonesho ya Nane Nane ya Wakulima yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.***

# BRELA, BPRA, COSOTA, COSOZA wasaini makubaliano ya ushirikiano

*Na Christina Njovu na Nehemia Mihayo*




***Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa (aliyeketi kushoto), Kaimu Mkurugezi wa Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), Bw. Rashid Masoud Othman (aliyeketi wa pili kutoka kushoto), Afisa Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) Bi. Doreen Sinare (aliyeketi wa pili kutoka kulia) na Mkurugenzi wa Idara ya Leseni, Ukaguzi na Ugawaji Mirabaha kutoka Taasisi ya Hakimiliki Zanzibar (COSOZA), Bw. Muumin Mwinyi Mzee (aliyeketi kulia) wakisaini makubaliano ya ushirikiano yenye lengo la kutekeleza mradi wa Kituo cha Mafunzo ya Miliki Ubunifu nchini, tarehe 21 Julai, 2023 jijini Dar es Salaam.***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesaini makubaliano ya ushirikiano baina yake na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) na Ofisi ya Hakimiliki Zanzibar yenye lengo la kutekeleza mradi wa Kituo cha Mafunzo ya Miliki Ubunifu nchini.

Hayo yalijiri tarehe 21 Julai, 2023 mbele ya aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Balozi, Dkt. Pindi Chana katika hafla ya ugawaji mirabaha kwa wabunifu iliyofanyika kwenye Hoteli ya Hyatt Regency, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alibainisha kuwa Serikali inatambua uhitaji mkubwa wa elimu na mafunzo kuhusu Miliki Ubunifu ili kuhakikisha kuwa bunifu zinaendelea kufanyika, zinalindwa na zinaingiza kipato stahiki kwa wabunifu.

"Uanzishwaji Kituo cha Mafunzo ya Miliki Ubunifu hapa nchini ni dhamira ya dhati ya Serikali katika kuhakikisha wabunifu wananufaika na kazi zao lakini pia zinalindwa. Mafunzo haya yatatolewa kwa wasanii, waandishi na wabunifu wote katika masuala ya Hakimiliki na masuala ya Miliki Ubunifu kwa ujumla", alisema Bw. Nyaisa.

Awali, BRELA ikiwa ni Ofisi ya Miliki Ubunifu kwa kushirikiana na COSOTA, COSOZA na BPRA ziliwasilisha maombi kwa Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO) ya uanzishwaji wa kituo hicho cha mafunzo.

Bw. Nyaisa aliongeza kuwa kwa sasa Tanzania na WIPO wanafanya utaratibu wa kufanya tathmini ya mahitaji nchini. Pia katika utekelezaji wa Mradi huu Taasisi zinazosimamia masuala ya Miliki Ubunifu zitatoa wataalam ili kuwezesha utoaji wa mafunzo husika.

Aliwapongeza wabunifu wote kwa kuendelea kufanya kazi na kubuni kazi mbalimbali za ubunifu katika sanaa na kazi za maandishi na kuhakikisha kuwa wanajipatia kipato na Taifa kwa ujumla.

Utolewaji wa mafunzo haya nchini Tanzania utasaidia kuhamashisha wabunifu kufanya bunifu nyingi zaidi, kuipandisha Tanzania kwenye ramani katika masuala hayo na kuwa chachu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.



***Aliyekuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akiwa na Naibu Waziri Mhe. Hamis Mwinjuma wakifuatilia utiwaji saini makubaliano ya ushirikiano kwa ajili ya utekelezaji wa Kituo cha Mafunzo ya Miliki Ubunifu nchini, hafla iliyofanyika katika Hoteli ya Hyatt Regency, jijini Dar es Salaam.***

# Waziri Gwajima awataka wajasiriamali kurasimisha biashara zao




***Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima akifungua Kongamano la Wanawake na Ununuzi wa Umma lililoandaliwa na Taasisi ya Ng'arisha Maisha Foundation na kufanyika tarehe 24 Agosti, 2023 jijini Tanga.***

*Na Peter Tweve*

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima aliwataka wajasiriamali kurasimisha biashara zao ili waweze kufanya biashara kwa wigo mpana zaidi.

Dkt. Gwajima aliyasema hayo tarehe 24 Agosti, 2023 katika ufunguzi wa Kongamano la Wanawake na Ununuzi wa Umma lililoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la Ng'arisha Maisha Foundation Jijini Tanga, lenye lengo la kutoa mwamko kwa wajasiriamali ili waweze kuchangamkia fursa mbalimbali zinazopatikana baada ya kurasimisha biashara zao.

Aliongeza kuwa ili kwenda na wakati na kupata fursa zinazotokea katika mchakato mzima wa ununuzi ni vyema wajasiriamali wakarasimisha biashara zao ili kuwa miongoni mwa watakaopata zabuni.

"Natambua kuwa mmekuwa mkiandaa bidhaa bora na wengine mkiwa na huduma ambazo kwa namna moja au nyingine mnapaswa kupata zabuni ila pasipo kurasimisha biashara zenu BRELA na taasisi nyingine itakuwa ni vigumu kupata nafasi hizi, hivyo mfike kurasimisha biashara zenu", alisema Dkt. Gwajima.

Kwa upande wake Afisa Usajili kutoka BRELA Bw. Abdul Songoro akifafanua kuhusu huduma zinazotolewa na na Taasisi katika Kongamano hilo alisisitiza kuwa milango ya kufungua biashara ipo wazi na BRELA imerahisisha huduma kwani wanaweza kujisajili mahali popote walipo kupitia Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS).

Alisisitiza kuwa BRELA inaendelea kuwasogezea wadau huduma ikiwa ni pamoja na kuwafikia mahali popote ili kutoa mafunzo na huduma za papo kwa papo.

Wajasiriamali zaidi ya 1,000 walihudhuria Kongamano hilo na kuonesha mwitikio mkubwa katika kuchangamkia fursa hasa za kusajili biashara zao.



***Baadhi ya washiriki wa Kongamano la Wanawake na Ununuzi wa Umma wakimsikiliza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima wakati wa ufunguzi wa Kongamano hilo lililofanyika jijini Tanga.***

# BRELA yawanoa wauzaji wa mazao ya kilimo

***Na Nehemia Mihayo***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) tarehe 24 Agosti, 2023 ilitoa mafunzo maalum kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi jijini Arusha yenye lengo la kuwajengea uwezo ili kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu urasimishaji biashara.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Bw. Ramadhani Madeleka alieleza kuwa wafanyabiashara wanatakiwa kutumia fursa hii ya kipekee iliyotolewa na serikali kuhakikisha changamoto zao zinatatuliwa.

"Mafunzo haya ni matokeo ya changamoto ambazo mlimueleza Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akiwa ziarani katika Jiji la Arusha, hivyo Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwa Ofisi ya RAS na BRELA kufanya mafunzo wezeshi kwenu ili kuzimaliza changamoto hizo. Tumieni fursa hii vizuri", ameeleza Bw. Madeleka.

Bw. Madeleka alipongeza BRELA kwa kuwa chachu ya uanzishwaji, urasimishaji, na uboreshaji wa biashara hapa nchini ikiwa ni pamoja na kuwa kielelezo katika utekelezaji wa uboreshaji wa mazingira wezeshi ya ufanyaji Biashara hapa nchini.

Naye Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Isdor Nkindi ambaye ni Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni, alieleza kuwa dhima kuu ya mafunzo haya ni kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara kwa kukidhi matakwa ya sheria.

"Kundi hili ni miongoni mwa makundi mengi ya wafanyabiashara ambayo yatafikiwa na BRELA. Lengo kuu ni kuwasaidia wafanyabiashara wanaouza mazao ya kilimo nje ya nchi kujirasimisha kwa kuwa na Usajili wa Jina la Bishara au Kampuni, kuwa na nembo katika bidhaa zao ambazo zimesajiliwa na kuwa na Leseni za Biashara kundi "A" hatua itakayowawezesha kufanya biashara bila kukwama sehemu yeyote", ameeleza Bw. Nkindi.



***Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Bw. Ramadhani Madeleka (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo yaliyotolewa na BRELA jijini Arusha, kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi, tarehe 24 Agosti, 2023.***

Katika mafunzo hayo ya siku tatu, mbali na kutoa elimu pia huduma ya usajili wa papo kwa papo zilitolewa kwa wafanyabiashara wote ambao walikidhi vigezo.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo Bi. Agness Mushi alisema mafunzo hayo yamemsaidia kutambua urahisi wa kurasimisha biashara tofauti na awali.

"Awali nilikua naogopa kuomba Leseni ya Biashara kundi "A", Jina la Biashara au Kampuni kwa kuhofia kubanwa na sheria pamoja na gharama, mafunzo haya yamenifanya nione sheria hizi ni rafiki na gharama za Usajili sio kubwa", alisema Bi. Mushi.

Mafunzo hayo yalifanyika ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali yaliyotolewa tarehe 1 Agosti, 2023 na Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji akiwa ziarani jijini humo. Mafunzo kama hayo pia yalifanyika mkoani Kilimanjaro kuanzia tarehe 28 hadi 30 Agosti 2023.



***Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Bw. Ramadhani Madeleka ( aliyesimama) akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi yaliyofanyika tarehe 24 Agosti, 2023 jijini Arusha.***

# BRELA yapongezwa kwa huduma bora

*Na Gloria Mbilimonywa*

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe (Mb), kwa mara nyingine tena, ameipongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kwa uboreshaji wa huduma za urasimishaji biashara nchini.

Pongezi hizo alizitoa tarehe 28 Agosti, 2023 wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki, katika viwanja vya Furahisha Jijini Mwanza.

"BRELA mnafanya kazi nzuri sana hasa katika urasimishaji wa biashara nchini, naomba muendelee kuboresha huduma na kasi zaidi ili kuwafikia wateja wengi zaidi", alisema Mhe. Kigahe

Maonesho haya ya siku kumi ambayo yalishirikisha washiriki kutoka nchi za Tanzania, Uganda na Kenya yalianza tarehe 25 Agosti, 2023 na kuhitimishwa tarehe 3 Septemba,2023.




***Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe (Mb.) akisikiliza maelezo kutoka kwa Afisa wa BRELA (hayupo pichani) alipotembelea banda la Taasisi hiyo wakati wa Maonesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza.***




*Afisa wa BRELA Bw. Francis Filimbi akimkabidhi cheti cha usajili wa Jina la Biashara mdau aliyefika katika banda la BRELA kupata huduma za usajili wa papo kwa papo wakati wa Maonesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika viwanja vya Furahisha jijini Mwanza.*




***Mmoja wa wananchi waliofika katika banda la BRELA kusajili jina la biashara wakati wa maonesho ya 18 ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika viwanja vya Furahisha jijini Mwanza.***

# BRELA kumaliza dukuduku la wauzaji mazao nje ya nchi


***Na Nehemia Mihayo***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Agosti 28, 2023 ilizindua mafunzo maalum kwa wafanyabiashara wanaouza mazao nje ya nchi waliopo Mkoa wa Kilimanjaro.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dkt. Vedast Makota alieleza kuwa BRELA pamoja na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa huo wamejipanga vizuri kwa ajili ya zoezi hilo.

"Leo timu ya wataalam kutoka BRELA ikishirikiana na ofisi ya RAS Kilimanjaro wapo hapa kujibu dukuduku zenu kuhusu manufaa ya urasimishaji biashara ikiwa ni pamoja na usajili wa Kampuni, Majina ya Biashara na Leseni za Biashara Kundi "A"," alisema Dkt. Makota.

Aidha, alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imedhamiria kujenga uchumi wenye tija kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wafanyabiashara wa aina zote kujua umuhimu wa kufanya biashara ndani ya mfumo



***Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni kutoka BRELA Bw. Isdor Nkindi akitoa usaidizi wa kusajili kampuni papo kwa papo kwa mmoja wa washiriki wa mafunzo ya kujenga uwezo kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro.***



***Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni kutoka BRELA Bw. Isdor Nkindi akiwasilisha mada wakati wa mafunzo kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi yaliyofanyika tarehe 28 Agosti, 2023 mkoani Kilimanjaro.***

> *"Leo timu ya wataalam kutoka BRELA ikishirikiana na Ofisi ya RAS Kilimanjaro wapo hapa kujibu dukuduku zenu kuhusu manufaa ya urasimishaji biashara ikiwa ni pamoja na usajili wa Kampuni, Majina ya Biashara na Leseni za Biashara Kundi "A".*

Na Nehemia Mihayo

rasmi wa uchumi Tanzania.

Dkt. Makota alitoa rai kwa wafanyabiashara hao kuzingatia sheria, taratibu na kanuni katika majukumu yao kwakuwa Serikali ipo kwa ajili ya kuwezesha na itaendelea kuwezesha.

"Rai yangu kwenu ni kuwa wasikivu ili mjipatie yale mnayohitaji na kuboresha shughuli zenu kwa manufaa yenu na taifa zima. Tunatambua ninyi ni wafanyabiashara makini, wazalendo, na mnaojituma", alisema Dkt. Makota.

Akizungumza kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Kampuni, Bw. Isdor Nkindi alieleza kuwa Dira ya Taasisi ni kuweka mazingira rafiki ya biashara nchini kwa kurasimisha biashara na kulinda Miliki Ubunifu kupitia Usajili na utoaji wa Leseni.

"Mafunzo haya ni utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji aliyotoa Agosti 1, 2023. Katika kutekeleza agizo hilo BRELA imefika hapa kwa ajili ya kuwapa mafunzo maalumu ya siku tatu kwa wadau hawa kuanzia Agosti 28, hadi 30, 2023. Nina imani wadau hawa watakuwa mabalozi wazuri katika maeneo yao ya kazi", alisema Bw. Nkindi.




***Mshiriki wa mafunzo yaliyotolewa na BRELA kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi akipata usaidizi wa usajili kwa kutumia simu yake ya kiganjani ili kujithibitishia jinsi BRELA ilivyorahisisha upatikanaji wa huduma zake kwa njia ya mtandao***

> *"Rai yangu kwenu ni kuwa wasikivu ili mjipatie yale mnayohitaji na kuboresha shughuli zenu kwa manufaa yenu na taifa zima. Tunatambua ninyi ni wafanyabiashara makini, wazalendo, na mnaojituma".*




***Mmoja wa wadau walioshiriki mafunzo yaliyoandaliwa na BRELA kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi akisaidiwa na Kaimu Mkuu wa sehemu ya majina ya Biashara Bw. Harvey Kombe kusajili kampuni papo kwa papo wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika tarehe 26 Agosti, 2023 mkoani Kilimanjaro.***



***Mmoja wa washiriki wa mafunzo ya kujenga uwezo kwa wauzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi akisaidiwa na Afisa wa BRELA Bw. Peter Riwa kuandaa maombi ya usajili kwa njia ya mtandao wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika mkoani Kilimanjaro.***

# BRELA yashiriki jukwaa la AGRF 2023

**Na Roida Andusamile**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeshiriki katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (Africa Food Systems Forum - AGRF), kwa kutoa elimu ya urasimishaji biashara kwa washiriki wa Jukwaa hilo.

BRELA ilishiriki ikiwa na banda lake ndani ya banda la Wizara ya Viwanda na Biashara, ambapo ilitoa elimu juu ya huduma zote za BRELA ikiwa ni pamoja na Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Kampuni, Alama za Biashara na Huduma, Utoaji Hataza pamoja na Leseni za Viwanda na za Biashara Kundi “A”.




*Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando akiwa na Afisa wa BRELA Bi. Gift Wazingwa wakitoa huduma kwa mteja wakati wa Jukwa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam*

Akizungumza na Waandishi wa Habari katika Jukwaa hilo Septemba 5, 2023 Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe aliwataka Watanzania kutumia Jukwaa hilo la AGRF linalofanyika Jijini Dar es Salaam kama fursa ya kuijulisha dunia rasilimali zilizopo nchini na namna gani Watanzania watashiriki kuzitumia ili waweze kufanya biashara na mataifa mengine duniani na hasa biashara ya chakula kwa kuwa dunia inatarajia kuwa na watu bilioni tisa ifikapo mwaka 2030, ambapo kwa Bara la Afrika inakadiriwa kufikia watu bilioni mbili, na Tanzania watu milioni 80 ambao wote wanahitaji chakula.

“Kufanyika kwa Jukwaa hili hapa nchini, kutatatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima kwa kuwa kilimo kinahitaji fedha, na pia uwekezaji wa kumsaidia mkulima mdogo ama mkubwa, hivyo jukwaa hili limewaleta pamoja wawekezaji mbalimbali ambao watawezesha wakulima kwa mitaji”, alifafanua Mhe. Bashe.

Jukwaa hilo lililofanyika kwa siku nne liliandaliwa na Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (Africa Food Systems Forum), ambalo liliwakutanisha wadau kujadili kwa pamoja hatua za kuboresha kilimo na mifumo ya chakula barani Afrika.




*Afisa wa BRELA Bi. Gift Wazingwa akimsikiliza mteja aliyefika katika banda la BRELA kupata huduma wakati wa Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) ukiendelea katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam*

> “Kufanyika kwa Jukwaa hili hapa nchini, kutatatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima kwa kuwa kilimo kinahitaji fedha, na pia uwekezaji wa kumsaidia mkulima mdogo ama mkubwa, hivyo jukwaa hili limewaleta pamoja wawekezaji mbalimbali ambao watawezesha wakulima kwa mitaji”.

# Watumishi BRELA wapatiwa elimu kuhusu NHIF, UTT, Watumishi Housing, Vyama vya Ushirika

**Na Roida Andusamile**

Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wamepatiwa elimu kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko wa Uwekezaji (UTT) na Watumishi Housing Investments ili waweze kuelewa na kutumia huduma na fursa zinazotolewa na taasisi hizo ipasavyo.

Akifungua mafunzo hayo tarehe 9 Septemba, 2023 katika ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii, jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Huduma na Uwezeshaji wa BRELA, Bw. Daimon Kisyombe alieleza kuwa mafunzo hayo kwa watumishi wa BRELA yamelenga kuwapa uelewa kuhusu huduma muhimu za afya zinazotolewa kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na taratibu za kuzingatia ili kupata huduma hizo na kuwapa elimu kuhusu fursa mbalimbali za uwekezaji zinazotolewa na Taasisi za Umma ili kuwajengea watumishi utamaduni wa kuwekeza kwa ustawi wao pia kama sehemu ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu.

Pamoja na mafunzo hayo, watumishi walipata fursa ya kupewa elimu ya Ushirika ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuanzisha Chama cha Akiba na Mikopo kwa watumishi wa BRELA ili kupanua wigo kwa watumishi kuboresha maslahi yao na kupata fedha za kuwasaidia katika kujenga maisha yao ya sasa na baadaye.

Kupitia mafunzo hayo, watumishi walipata fursa ya kupitia na kuidhinisha Katiba ya Chama na kuteua uongozi na kamati muhimu kwa ajili ya kukamilisha taratibu za usajili wa Chama.

Akiwasilisha mada kuhusu huduma za NHIF Afisa kutoka taasisi hiyo Bi. Ridhia Makono alisema mfuko huo umekuwa ukihakikisha kuwa mwanachama anahudumiwa kulingana na michango inayotolewa na mwajiri kwa ajili ya matibabu. Aliwataka watumishi kuzingatia miongozo inayotolewa na mwajiri kuhusu matumizi ya huduma za ziada zinazogharamiwa na mwajiri na kuepuka gharama zisizo za lazima zinazotokana na mambo yasiyohusiana na matibabu (lifestyle issues).

Kwa upande wake Afisa Mwandamizi kutoka Watumishi Housing Bw. Pascal Masawe alisema mtumishi anatakiwa kuwekeza kuanzia sasa kwa kununua nyumba na viwanja kwa bei nafuu na kulipa kidogo kidogo mpaka hapo atakapokamilisha malipo na kuwa mmiliki halali wa nyumba au kiwanja.

Aidha,Bw. Masawe aliwahamasisha watumishi kuchangamkia fursa ya kuwekeza katika mfuko wa Faida Fund kwa kununua vipande ambavyo thamani yake imekuwa ikiongezeka kwa haraka kwani katika kipindi cha miezi tisa (9) thamani ya kipande imeongezeka kutoka TZS 100 kipindi cha Januari, 2023 hadi kufikia TZS 106.9 kipindi cha Septemba, 2023.

Naye Afisa Mwandamizi kutoka UTT AMIS Bw. Rahim Mwanga, aliwasilisha mada kuhusu umuhimu na faida za kuwekeza katika mifuko iliyoanzishwa na UTT AMIS. Pia alifafanua kuhusu viwango vya uwekezaji na aina ya mifuko ambayo ni Umoja, Mfuko wa watoto, Mfuko wa Kujikimu, pamoja na Mfuko wa Ukwasi na kuwashauri watumishi kujiunga na mifuko hiyo ili kuwa washirika katika uwekezaji ambao utaleta tija katika maisha yao.

Mafunzo hayo yalikuwa ni mwendelezo wa mafunzo yanayotolewa na BRELA kwa watumishi wake ili kuwajengea uelewa wa pamoja kuhusu masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kuzingatia Sheria na kanuni za utumishi wa umma ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuchangamkia fursa mbalimbali za uwekezaji zinazotolewa na taasisi nyingine za Serikali.




*Mtumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Malema Siwakwi akichangia mada baada ya wasilisho kutoka kwa Afisa wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Bi. Ridhia Makono wakati wa mafunzo kwa watumishi wa Taasisi yaliyofanyika tarehe 9 Septemba 2023 katika ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dar es Salaam.*



*Afisa kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Bi. Ridhia Makono akiwasilisha mada kuhusu huduma za mfuko huo kwa watumishi wa BRELA walioshiriki mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyofanyika tarehe 9 Septemba, 2023 katika ukumbi wa Chuo cha Taifa cha Utalii.*

# BRELA yatoa huduma za sajili maonesho ya wajasiriamali "Imbeju"

***Christina Njovu***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeshiriki katika Maonesho ya Wajasiriamali "Imbeju" na kutoa huduma za papo kwa papo za sajili mbalimbali jijini Dar Es Salaam.

Maonesho hayo ya siku tatu yaliyoandaliwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa kushirikiana na Benki ya CRDB, yalifunguliwa rasmi tarehe 11 Septemba, 2023 na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Wenye Mahitaji Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb) katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Katika maonesho hayo wajasiriamali wanaozalisha bidhaa mbalimbali walijitokeza kwa wingi kuonesha na kuuza bidhaa hizo huku taasisi za Serikali zikishiriki kwa kutoa huduma na elimu kwa wadau waliotembelea maonesho hayo.

Aidha, BRELA ilishiriki katika maonesho hayo na kutoa huduma kwa wadau waliotembelea banda hilo kwa kuwapatia elimu kuhusu huduma zinazotolewa na Taasisi ikiwa ni pamoja na Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Kampuni, Usajii wa Alama za Biashara na Huduma na jinsi ya kupata Leseni za Biashara kundi "A".

Maonesho hayo ya siku tatu (3) yalihitimishwa Jumatano tarehe 13 Septemba, 2023.

> "Sajili Ubunifu wako upate ulinzi wa Kisheria".



***Msaidizi wa Usajili wa BRELA Bw. Athuman Makuka (kulia), akitoa elimu juu ya Usajili wa Alama ya Biashara na Huduma kwa mdau aliyetembelea banda la BRELA katika Maonesho ya Wajasiriamali (Imbeju), yaliyofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja Jijini Dar es Salaam.***



***Afisa TEHAMA wa Wakala wa BRELA Bi. Mwanaisha Mmari (kulia), akitoa usaidizi wa usajili wa Jina la Biashara kwa wadau waliotembelea banda la BRELA katika maonesho ya Wajasiriamali (Imbeju), yaliyohitimishwa tarehe 13 Septemba,2023 katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Jijini Dar es Salaam.***

# BRELA yashiriki katika Maonesho ya 6 ya Teknolojia ya Madini mjini Geita

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ilishiriki katika Maonesho ya sita (6) ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini ya mwaka 2023, kwa kutoa elimu na huduma mbalimbali za sajili na utoaji wa Leseni. Maonesho hayo yalifanyika katika viwanja vya Bombambili mjini Geita kuanzia tarehe 20 Septemba, hadi 30 Septemba, 2023.

Banda la BRELA lilikuwa miongoni mwa mabanda ya taasisi za serikali ambazo zilishiriki katika maonesho hayo ya madini, BRELA ilitumia jukwaa la maonesho hayo kuhamasisha wadau mbalimbali kurasimisha biashara zao pamoja na kutoa usaidizi kwa wadau wanaopata changamoto katika mfumo wa usajili kwa njia ya Mtandao - ORS

Pamoja na kutoa elimu kwa umma na usaidizi, BRELA pia ilitoa huduma zote za usajili na utoaji Leseni papo kwa papo. Huduma hizo ni pamoja na usajili wa Majina ya Biashara, Kampuni, Alama za Biashara na Huduma, utoaji wa Leseni za biashara kundi "A", Usajili wa Viwanda, utoaji wa Hataza, na huduma za kulipia ada za mwaka na uhuishaji wa taarifa za kampuni.

Maonesho hayo yalitarajiwa kufunguliwa rasmi tarehe 23 Septemba, 2023 na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Doto Biteko na kufungwa tarehe 30 Septemba, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.



***Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Majina ya Biashara Bw. Harvey Kombe, akitoa elimu kwa mmoja wa wadau waliofika katika banda la BRELA kupata huduma wakati wa Maonesho ya 6 ya Teknolojia ya Madini mjini Geita.***



***Maafisa wa BRELA, wakitoa elimu na huduma ya papo kwa papo kwa wadau waliotembelea banda la BRELA katika viwanja vya Maonesho ya 6 ya Kimataifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika katika Viwanja vya Bombambili mjini Geita.***

# Maafisa wa BRELA watakiwa kuzingatia maadili

*Na Peter Tweve*



***Maafisa wa BRELA wakishiriki mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya kuandaa mashauri na kutoa ushahidi mahakamani yaliyofanyika katika Ukumbi wa APC Bunju, jijini Dar es Salaam.***

Maafisa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), kutoka Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara na Kurugenzi ya Miliki Ubunifu wametakiwa kuzingatia maadili na kufanya kazi kwa weledi ili kufanikisha malengo waliyojiwekea.

Hayo yalisemwa katika mafunzo yaliyoendelea katika ukumbi wa APC Bunju "A" Kinondoni, Jijini Dar es Salaam, ya kuwajengea uwezo maafisa hao kuhusu namna ya kuandaa mashauri ambayo BRELA inatakiwa kushiriki Mahakamani kutoa ushahidi wa kesi mbalimbali.

Akiwasilisha mada katika mafunzo hayo, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu, Mhe. Jaji Robert Makaramba aliwataka kuzingatia namna ya kuandaa mashauri na kujiepusha na vitendo ambavyo vitasababisha kesi mbalimbali kuchelewa.

Pia aliwataka kutojihusisha na vitendo ambavyo vitasababisha kuhujumu mwenendo wa mashauri mbalimbali ambayo msingi wake ni kutoa haki, ambapo maafisa wa BRELA hushiriki katika kutoa ushahidi mbalimbali kwa kesi ambazo Taasisi huitwa mahakamani.

"Mnatakiwa kuzingatia namna ya kuandaa mashauri vizuri na vilevile baada ya kutoka katika kesi hizo, zikiwa bado hazijaamuliwa mjiepushe na kuyaongelea yanayoendelea Mahakamani ili kutohujumu mienendo ya kesi hizo", alisema Mhe. Jaji Makaramba.

Pia alihimiza kuwa na ushirikiano na kuwa na ari ya kujifunza kila wakati ili kufahamu namna ya kuiwakilisha vyema Taasisi wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalianza Septemba 20 na kuhitimishwa Septemba 22, 2023, yaliwahusisha moja kwa moja maafisa wanaotakiwa kushiriki katika mashauri mbalimbali Mahakamani kwa lengo la kuwajengea uwezo na umakini ili waweze kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

> *"Mnatakiwa kuzingatia namna ya kuandaa mashauri vizuri na vilevile baada ya kutoka katika kesi hizo, zikiwa bado hazijaamuliwa mjiepushe na kuyaongelea yanayoendelea Mahakamani ili kutohujumu mienendo ya kesi hizo".*




***Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu Mhe. Dkt. Robert Makaramba akitoa mada katika mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa wa BRELA***

Wakiendelea na mafunzo hayo yaliyojikita katika uandishi sahihi wa maamuzi yanayotolewa na Baraza la Usuluhishi la Alama za Biashara na Huduma, Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu Mhe. Jaji Dkt. Fauz Twaib aliwataka maofisa hao kuzingatia namna bora ya kuandaa maandiko yanayotokana na maamuzi yanayotolewa na Mahakama ili kutenda haki.

Mhe. Jaji Dkt. Twaib aliwataka maofisa hao kuwa makini na kuzingatia weledi wa jinsi kuandika maamuzi ili Taasisi kuwa kioo kwa jamii.




BRELA tanzania   Brela _tanzania   brela _tanzania   brela _tanzania

# BRELA yapiga kambi ya huduma jumuishi uwanja wa Maonesho wa Mwalimu J.K. Nyerere



*Afisa Sheria BRELA Bw. Andrew Malesi (mwenye suti ya Bluu), akitoa elimu kuhusu usajili wa Alama za Biashara na Huduma, kwa wanachama wa Shirikisho la Vikundi vya Kijamii mkoa wa Dar es Salaam (TFUP), waliotembelea Banda la BRELA kupata elimu ya namna wanavyoweza kusajili Biashara zao na kupata Leseni, ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za ujasiriamali. (wa tatu kushoto), ni Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano (BRELA), Bi. Roida Andusamile.*

Katika maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar Es Salaam, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilijizatiti na kuweka kambi katika maonesho hayo. Kwa maonesho ya mwaka huu BRELA ilitenga maeneo manne tofauti kuwawezesha wananchi kupata huduma katika mabanda yao kwa wakati, kulingana na mahitaji yao.

Hatua hii ilitokana na uzoefu uliopatikana katika maonesho yaliyopita ambapo wananchi walimiminika kwa wingi katika banda la BRELA kupata elimu na huduma mbalimbali zilizokuwa zikitolewa ikiwemo kusajili majina ya biashara, kupata leseni na huduma zingine baada ya sajili.

Maeneo hayo yaliyotengwa na BRELA ni pamoja na Banda la huduma za Miliki Ubunifu, banda lingine lilitoa huduma jumuishi, na mabanda mengine mawili yalitoa huduma za usajili wa papo kwa hapo.



*Afisa Sheria, Kurugenzi ya Miliki Ubunifu Bw. Calvin Rwambogo akitoa elimu kwa wadau waliotembelea banda la BRELA la Miliki Ubunifu wakati wa maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam.*



*Msaidizi wa Usajili Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara Bi. Maryglory Mmari (kulia), akitoa elimu ya usajili wa majina ya Biashara na kampuni kwa wanachama wa Shirikisho la Vikundi vya Kijamii Mkoa wa Dar es Salaam (TFUP) waliofika katika banda la BRELA kupata elimu kwenye maonesho ya Saba Saba jijini Dar es Salaam wa pili kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano BRELA Bi. Roida Andusamile.*

## Mkuu wa Mkoa wa Njombe Atembelea Banda la BRELA Viwanja vya John Mwakangale, Mbeya

Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka tarehe 4 Agosti, 2023 alitembelea banda la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika Maonesho ya Kimataifa ya Wakulima (Nane Nane) yaliyofanyika katika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya. Mhe. Mtaka ameitaka BRELA kuongeza jitihada katika kuhamasisha wadau kurasimisha biashara zao ili kukuza uchumi wa nchi.



***Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Godfrey Nyaisa, (wa pili kushoto), akitia saini katika kitabu cha wageni alipotembelea Banda la Chuo Kikuu Mzumbe, kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo Nanenane katika Viwanja vya John Mwakangale Agosti 7, 2023Jijini Mbeya.***




***Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka akipata maelezo kuhusu wageni waliotembelea banda la BRELA.***




***Mkuu wa Mkoa wa Njombe Mhe. Anthony Mtaka akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa BRELA walioshiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Nane Nane kwenye viwanja vya John Mwakangale, Mbeya.***

# Maonesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki, Mwanza 2023



*Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Ukerewe Bi. Neema Mgobella alipotembelea banda la Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na kujionea jinsi watumishi wa Taasisi hiyo wanavyotoa huduma za papo kwa papo katika Maonesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika katika uwanja wa Furahisha jijini Mwanza.*









*Maafisa wa BRELA wakihudumia wateja waliofika katika banda la BRELA kupata huduma za usajili wakati wa Maonesho ya 18 ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza.*

# Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya St. Joseph Cathedral wafanya ziara ya mafunzo BRELA

*Wanafunzi wa Kidato cha Sita kutoka Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Joseph (St. Joseph Cathedral), ya Jijini Dar es Salaam Septemba 08, 2023 walifanya ziara ya mafunzo katika Ofisi za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na kupatiwa elimu kuhusu urasimishaji wa biashara. Wanafunzi hao wanaosoma mchepuo wa Biashara walielimishwa juu ya Usajili wa Majina ya Biashara, Usajili wa Kampuni Usajili wa Alama za Biashara na Huduma, utoaji wa Leseni za Biashara Kundi "A" na Utoaji wa Leseni za Viwanda.*

*Ziara ya wanafunzi hao ni mwendelezo wa Taasisi katika kuwapatia elimu wanafunzi wa sekondari na vyuo vikuu wenye lengo la kuwawezesha kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA*



*Afisa wa BRELA kutoka Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara, Bw. Yusufu Mwasakafyuka akizungumza na wanafunzi wa mchepuo wa biashara kutoka Shule ya Sekondari ya St. Joseph Cathedral walipotembelea Ofisi za BRELA kujifunza kuhusu*











*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa katika picha ya pamoja na watumishi wa Chuo Kikuu Mzumbe alipotembelea banda la chuo hicho wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Nane Nane jijini Mbeya*

## BRELA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA CHUO KIKUU MZUMBE

Hivi karibuni Wakala wa usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilifanya kikao na Chuo Kikuu Mzumbe. Kikao hicho kilichofanyika tarehe18 Agosti, 2023 katika Ofisi za BRELA kujadili kuhusu kuimarisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu baina ya Chuo hicho na BRELA hasa katika masuala ya Miliki Ubunifu na urasimishaji wa biashara.



*Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Andrew Mkapa (kulia) akimkabidhi zawadi Rais wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya, Prof. Henry Mollel (kushoto) mara baada ya Kikao na Kurugenzi ya Miliki Ubunifu ilichofanyika katika Ofisi za BRELA Jijini Dar es Salaam tarehe 18 Agosti, 2023.*





# BRELA yatoa huduma za papo kwa papo Tamasha la Utamaduni Njombe

***Na Njwaba Mwaijibe***

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ilishiriki katika Tamasha la Pili la Taifa la Utamaduni mkoan Njombe kwa kutoa elimu na huduma za urasimishaji biashara za papo kwa popo.

Katika tamasha hilo BRELA ilitoa elimu kuhusu Usajili wa Majina ya Biashara, Kampuni, Alama za Biashara n Huduma, utoaji wa Hataza, Leseni za Biashara Kundi "A" na Leseni za viwanda.

Tamasha hilo lililoanza Agosti 25, 2023 katika viwanja vya stendi ya zamani mkoani hapo, lilihitimishwa Agost 27, 2023.

Kauli mbiu ya maonesho hayo ilikuwa ni "Utamaduni ni msingi wa maadili, tuulinde na kuendeleza".




***Msaidizi wa Usajili Mwandamizi kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Nassoro Mtavu akimpatia maelezo Mkurugenzi wa Kampuni ya Shambani GreenGold Limited, Bw. Mahendeka Jeremiah, kuhusu utaratibu wa kuhuisha taarifa za mwaka za Kampuni, alipotembelea banda la kliniki ya biashara kwenye Tamasha la Pili la Taifa la Utamaduni mkoani Njombe, ambalo lilihitimishwa Agosti 27, 2023.***

## Ofisi ya Hataza ya Japan (Japan Patent Office) kuanzisha ushirikiano na BRELA



***Baadhi ya watumishi wa Kurugenzi ya Miliki Ubunifu BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na Mwakilishi wa Ofisi ya Hataza ya Japan kwa nchi za Afrika na Mkurugenzi wa Shirika la Biashara za Nje la Japan (Japan External Trade Organization - JETRO), Bw. Keisuke Seki, alipotembelea Ofisi za BRELA tarehe 22 Agosti, 2023 jijini Dar es Salaam.***

# Wakutana kujadili mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa leseni za viwanda

*Na Roida Andusamile*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imekutana na wawakilishi kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar ili kujadili njia bora za uendeshaji wa mifumo ya kielektroniki ya utoaji wa Leseni za Viwanda kwa pamoja, katika utekelezaji wa Sheria ya Taifa ya Usajili na Leseni ya Viwanda ambayo ni ya Muungano.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa akifungua kikao hicho tarehe 25 Septemba, 2023 katika ofisi za BRELA jijini Dar es Saam amesema kikao hicho ni mwendelezo wa utekelezaji wa Maelekezo kuwa Watendaji kutoka Taasisi hizo za pande mbili za Muungano kukaa na kujadiliana kuhusu matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa pamoja utakaotumika katika utoaji wa Leseni za Viwanda ili pia kurahisisha upatikanaji wa Takwimu za Viwanda kwa pande zote mbili za Muungano.

Bw. Nyaisa alisema upande wa Tanzania Bara, Sheria ya Taifa ya Utoaji wa Leseni na Usajili wa Viwanda imekuwa ikitekelezwa kwa kutoa Leseni za Viwanda kwa viwanda vikubwa na Vyeti vya Usajili kwa Viwanda Vidogo licha ya Sheria hiyo kuwa na mapungufu kutokana na kutofanyiwa marekebisho kwa muda mrefu.



***Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajiliwa Biashara na Leseni (BRELA) Bw. Godfrey Nyaisa akifuatilia majadiliano wakati wa kikao cha pamoja na BRELA.***

Kwa upande wa Zanzibar, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda ambae ndiye aliyekuwa Mkuu wa Msafara kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Dkt. Abdullah R. Abdullah alisema Zanzibar katika utekelezaji wa Sheria hiyo inakusudia kutumia Mifumo ya kielektroni ya utoaji Leseni za Viwanda na Vyeti vya Usajili wa Viwanda vidogo itakayosomana kwa pande zote mbili za Muungano.

Dkt. Abdullah alibainisha kuwa katika utekelezaji wa Sheria hiyo Leseni za Viwanda na Vyeti vya Usajili vitakavyotolewa chini ya Sheria hiyo vinatakiwa kufanana kwa pande zote mbili za Muungano.

Aliendelea kubainisha kuwa itaangaliwa namna bora na rasmi itakayotumika katika ukusanyaji wa ada mbalimbali zinazolipwa chini ya Sheria hii.

BRELA na Idara ya Maendeleo ya Viwanda Zanzibar kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar wamekuwa wakikutana mara kwa mara kujadiliana kuhusu mapitio na maboresho ya Sheria ya Taifa ya Utoaji wa Leseni na Usajili wa Viwanda ambayo kwa ujumla wake, ambayo ilitungwa mwaka 1967, ili kuifanya iendane na hali halisi ya sasa.



***Baadhi ya watumishi wa BRELA na wajumbe kutoka Idara ya Maendeleo ya Viwanda Zanzibar wakifuatilia majadiliano wakati wa kikao hicho cha pamoja kilichofanyika tarehe 25 Septemba, 2023 katika Ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.***

# Wavumbuzi wa dawa na tiba asili kulindwa kisheria

Na Lugano Mwakyombe

Wavumbuzi wa dawa na tiba mbalimbali asilia wamehimizwa kufuata taratibu za kulinda vumbuzi zao kisheria ili ziweze kuwanufaisha.

Hayo yalibainishwa Septemba 26, 2023 katika ukumbi wa Holiday Inn Jijini Dar es Salaam, katika Mafunzo ya uthibiti na kulinda Tiba Asilia yanayo simamiwa na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO).

Akitoa neno la ufunguzi Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Alama za Biashara na Huduma Bw. Seka Kasera, kwa niaba ya Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu, aliwataka washiriki ambao ni wavumbuzi wa tiba asilia kuhakikisha kwamba wanasajili vumbuzi zao ili kuzilinda kisheria.

Alisisitiza kuwa vumbuzi zinazohusu tiba mbadala kama vile dawa asilia ni muhimu kwa afya ya binadamu, hivyo lazima zitambuliwe na kurasimishwa kwa kuzisajili kama Hataza, Alama za biashara ama huduma. Hii itaongeza pato la Taifa kwa kutoa ajira kwa vijana na hatimaye kukuza uchumi wetu.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Afisa Sheria kutoka Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Bw. Calvin Rwambogo alisema kuwa uvumbuzi unaofanyika katika eneo hili ni muhimu kwa mvumbuzi pamoja na Taifa kwa ujumla.

"Watanzania wengi wanavumbua vitu mbalimbali lakini wanashindwa kunufaika na vumbuzi zao kwakuwa wengi wanakuwa hawajazisajili matokeo yake vumbuzi zao zinachukuliwa na wengine na wanazisajili", amesema Bw. Rwambogo.

Aidha alitoa wito kwa wavumbuzi hao kutambua nafasi ya BRELA



***Mtaalam wa Tiba Asilia kutoka MUHAS Prof. Esther Innocent akichangia mada wakati wa mafunzo ya udhibiti na kulinda tiba asilia yaliyosimamiwa na Shirika la Miliki Ubunifu Duniani (WIPO).***

Naye Mtaalam wa Tiba Asilia kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) Prof. aliwaasa wavumbuzi wa tiba asili kusajili hataza kupitia BRELA kwani hii ni faida kwao kutambulika rasmi pamoja na kuchangia uchumi wa Taifa kupitia bunifu hizo. Esther Innocent akichangia mada, katika kuzirasimisha na kulinda vumbuzi zao pamoja na umuhimu wa kulinda na kuhifadhi vumbuzi wanazozifanya katika kutatua changamoto mbalimbali za jamii.

Katika mafunzo hayo zaidi ya nchi kumi za Afrika zilishiriki kupitia njia ya Mtandao ambapo wachagiza Mada kutoka Geneva- Uswisi waliongoza mjadala huo.

BRELA imeshiriki na wadau wake mbalimbali wakiwemo Wataalamu wa Tiba Asilia kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, Tume ya Sayansi na Teknolojia, pamoja na taasisi zingine.

Mafunzo hayo yenye lengo la kuwajengea uwezo wadau hao maalum yalihitimishwa tarehe Septemba 27 2023.



***Washiriki wa mafunzo ya udhibiti na kulinda tiba asilia wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Holiday Inn jijini Dar es Salaam.***

# Miliki Ubunifu utajiri ambao usahaulika

*Na Stanislaus Kigosi*

Miliki Ubunifu, kama lilivyo neno lenyewe ubunifu ni dhana inayomaanisha mali isiyoshikika ambayo ni zao la matumizi ya akili ya binadamu katika kubuni, kuvumbua na kusanifu vitu mbalimbali. Ubunifu ni zao la fikra za binadamu. Ni kupitia fikra hizo binadamu anaibua mawazo ambayo huzalisha bidhaa na huduma ambazo hutumika katika maisha ya kila siku ya binadamu. Hivyo, kwa kiwango kikubwa chanzo cha utajiri na mali katika jamii ni ubunifu.




***Mmoja wa wabunifu akionesha baadhi ya bidhaa zake wakati wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam***

Dhana ya Miliki Ubunifu japokuwa katika mazingira ya Kiafrika bado inaonekana kuwa ngeni; lakini uhalisia wake ni kwamba Miliki Ubunifu zimekuwepo tangu dahari. Binadamu amekuwa akibuni na kuvumbua vitu na dhana mbalimbali tangu kale. Maendeleo ya jamii katika siasa, uchumi na teknolojia imekuwa ni chachu ya kuibadilisha dhana ya Miliki Bunifu kuja kuwa kama ambavyo inaeleweka na kufahamika leo hata kuundiwa sheria za kitaifa, kikanda na kimataifa ili kulinda haki za ubunifu unaofanywa na binadamu katika kukabiliana na mazingira.

Ni kupitia Miliki Ubunifu binadamu ameweza kuvumbua vitu mbalimbali na bidhaa mbalimbali ambazo zimemuwezesha kukabiliana na mazingira ya asili na kuboresha maisha yake na jamii inayomzunguka. Mashine na mitambo mbalimbali ni matokeo ya ubunifu wa binadamu. Mashine na mitambo hiyo inasaidia kukabiliana na changamoto kurahisisha kazi. Pia kupitia ubunifu madawa na vifaa tiba vimeweza kuvumbuliwa ili kuboresha afya ya binadamu pia kuboresha maisha ya




***Mbunifu Bi. Modesta Ogudu wa Kabinty Crafts akionesha bidhaa za mapambo ya majumbani wakati wa maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam.***

binadamu.

Maisha ya kila siku yamezungukwa na matumizi pia uzalishaji wa Miliki Bunifu wa aina mbalimbali. Lakini ni mara chache sana na pia ni watu wachache sana ambao hutambua kwamba wanatumia Miliki Ubunifu au wanazalisha Miliki Ubunifu ambazo hulindwa na sheria mbalimbali. Aghalabu katika kutimiza majukumu, watu wengi wamejikuta wakivunja haki za Miliki Ubunifu za watu wengine. Kuvunja haki zilizomo katika miliki bunifu ni kosa kisheria.

Mathalani, wafanyabiashara za maduka ya bidhaa za aina mbalimbali na wamiliki wa kumbi za burudani kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitumia kazi za sanaa bila kulipa fidia ya kutumia kazi zenye hakimiliki kwa wamiliki wa kazi hizo ambao ndiyo wenye haki ya kuamua kazi zao zitumike kwa namna gani na walipwe kiasi gani kwa mujibu wa sheria zinazolinda hakimiliki za kazi hizo kama muziki au kazi za filamu. Muziki au filamu zinaangukia kwenye kundi la miliki bunifu zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki. Bahati mbaya sana ni kwamba wamiliki kama ilivyo kwa watumiaji wa kazi hizo huwa hawana uelewa wa haki ambazo zimo ndani ya kazi hizo.

Miliki bunifu huzalisha siyo tu bidhaa bali huzalisha aina mbali mbali za huduma ambazo huwapa kipato wazalishaji wa bidhaa na huduma. Wazalishaji wengi wa bidhaa na watoa huduma katika nchi zinazoendelea Tanzania ikiwa ni mojawapo kitu pekee ambacho huwa wanakijali na kukipa thamani ni bidhaa au huduma anayoitoa. Wanasahau kulinda na kuupa thamani ule ubunifu uliomo ndani ya bidhaa na huduma zao.

Kama Miliki Ubunifu za wafanyabiashara na wazalishaji wa bidhaa na huduma wakizipa thamani na kuamua kuzilinda kwa mujibu wa sheria za nchi zinazosimamia ulizi wa miliki ubunifu, watakuwa wanaongeza siyo tu tija kwenye biashara katika bidhaa na huduma zao, bali pia watakuwa wanaongeza thamani ya aina mbalimbali ya biashara zao katika bidhaa na huduma wanazozalisha na kutoa kwa wateja wao.




***Afisa wa BRELA Bw. Andrew Malesi akiangalia ubunifu wa mashine ya umeme katika banda la Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT) wakati wa Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam katika Uwanja wa Maonesho Mwalimu J.K. Nyerere Barabara ya Kilwa, Temeke Dar es Salaam.***

Pia ulinzi wa miliki ubunifu kwa mujibu wa sheria husaidia kuwapa imani walaji na watumiaji wa bidhaa na huduma hizo mtawalia. Mmiliki wa alama ya biashara na huduma ambayo imeshapata ulinzi wa kisheria kwa kusajiliwa, anao uhakika mkubwa wa kuitumia alama yake ya biashara kupata mkopo hata kwenye taasisi za fedha na akaitumia alama yake ile kama dhamana ya mkopo wake au pia anaweza kuvutia wawekezaji wengine kwenye biashara yake ambao wataongeza mtaji wa biashara na hivyo kuongeza tija na ukuaji wa biashara husika.

Kwenye mazingira ya kawaida na kwa kuzingatia kuwa nchi nyingi zinazoendelea miliki bunifu hazikuwahi kupewa uzito na wafanyabiashara pamoja na wabunifu, lakini hili ni eneo ambalo wabunifu wengi na wamiliki wa ubunifu huo wamepoteza mapato na fursa za kukuza biashara zao. Naamini sasa ni wakati muafaka kwa wamiliki wa biashara na wajasiriamali kuona fursa inayotolewa na miliki bunifu katika kukuza biashara zao na huduma zao. Pia kupitia miliki bunifu fursa za kukuza teknolojia na uwekezaji wa kibiashara kwenye eneo la teknolojia, sanaa pamoja na utamaduni ambao utatochea kukuza utalii. Hivyo ieleweke kwamba miliki bunifu zinagusa maeneo yote ya kiuchumi na kibiashara, hii ni fursa iliyosahaulika kwa miaka mingi lakini ni eneo lenye utajiri mwingi.



***Washiriki wa mafunzo ya udhibiti na kulinda tiba asilia wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika Ukumbi wa Hoteli ya Holiday Inn jijini Dar es Salaam.***

# A CALL FOR COMPANIES TO FILE ANNUAL RETURNS

The Registrar of Companies calls all companies incorporated and in Tanzania to file their annual returns as required by the Companies Act, CAP 212.

## HOW TO FILE ANNUAL RETURNS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM

1. Log in on the Online Registration System (ORS).
2. Select e - service.
3. Select Company .
4. Select Filing of annual return (accounts) / Update.
5. Fill in Incorporation/Compliance number.
6. Fill in company's details.
7. Upload form 128 together with a signed and dated consolidated form and the . Financial Statement
8. Select m ode of payment (Mobile or Bank).
9. After payment the application will be received for review.

**Note:** Filing fee of an annual return is TZS.22,000.00 if submitted on time. Delayed submission of an annual return attracts a late filing fee of TZS.2,500.00 (compounded) per every month delayed or part thereof.

BRELA HOUSE, Plot No 23, Block No. 20,
Shaaban Robert Street/Sokoine Drive, P.O.Box. 9393, 11101 Ilala, Dar es Salaam,
Telephone: + 255 22 2212800, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz,
Website: www.brela.go.tz

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# CALL FOR FOREIGN COMPANIES TO FILE FINANCIAL STATEMENT

The Registrar of Companies calls all foreign companies with registered branches in Tanzania to submit their Financial Statements as required by the Companies Act, Cap 212.

## HOW TO FILE FINANCIAL STATEMENTS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM

Log in on the Online Registration System (ORS)

2. Select e service
3. Select Company
4. Select Filling of annual return(accounts)/update
5. Fill in Compliance number
6. Fill in Company's details
7. Upload audited financial satetement together with consolidated form
8. Click proceed button
9. An application will be received by Business Registrations and Licensing Agency (BRELA) for review and process
10. After the review and processing of an application, an invoice will be sent to the customer for payment of the required fee.

**Note:** Submission of financial statement costs USD,220.00 if submitted on time. Delayed submission of financial statements are charged USD,25.00 (compounded) per every delayed month.

BRELA HOUSE, Plot No 23, Block No. 20,
Shaaban Robert Street/Sokoine Drive, P.O.Box. 9393, 11101 Ilala, Dar es Salaam,
Telephone: + 255 22 2212800, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz,
Website: www.brela.go.tz

BRELA

WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI



Jengo la BRELA, Kitalu Na 20, Kiwanja Na 23
Mtaa wa Shaaban Robert / Barabara ya Sokoine, S.L.P. 9393,
Ilala, Dar es Salaam. Simu: +255-22 2212800,
barua pepe: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz ,

*Tovuti: www.brela.go.tz*

BRELA tanzania Brela _tanzania brela _tanzania +255 (0) 735 331 003 BRELA ONLINETV